

## **Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi**

[إِنَّ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدِقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهُ عَلَيْهِ فَإِنَّمَا مَنْ قَضَى نَحْبَهُ  
وَمِنْهُمْ مَنْ يَنْتَظِرُ وَمَا بَدَلُوا تَبْدِيلًا]

**“Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.” [Al-Ahzab:23]**  
**(Imetafsiriwa)**

Hisab ut Tahrir / Wilayah Uturuki yamuomboleza mmoja wa Mashababu wake waheshimiwa na watiifu,

## Nduqu Erkam Kılıçkaya

Ambaye alijitolea maisha yake kama Muislamu mkweli na mwenye ikhlasi katika kazi ya kurudisha mfumo kamili wa maisha ya Kiislamu, na pia aliyahitimisha katika da'wah. Pia, Erkam Kılıçkaya, ambaye alikuwa anaugua matatizo ya kiafya kwa miaka mingi, alikuwa na subira na maradhi haya na hakusita kubeba da'wah. Alijitahidi kwa ajili ya Uislamu kwa azma na shauku. [إِنَّ اللَّهَ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِحُونَ]  
**"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Munqu, na kwake Yeye hakika tutarejia."** [Al-Baqarah:156]

Tunashuhudia kwamba Erkam Kılıçkaya, mwenye umri wa miaka 30, alitumia maisha yake ili kuregea mfumo kamili wa maisha ya Kiislamu na kusimamisha Khilafah Rashida kwa niija ya Utume.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu ambariki ndugu yetu huyu kipenzi kwa rehema zake, na airuzuku familia yake subira na faraja, na tunatoa rambirambi kwa jamaa zake, vipenzi na ndugu zake katika dawah.

## Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Uturuki